# HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

## RISALA YA UPANDAJI MITI KI-WILAYA 2018/19

**Ndugu mgeni rasmi,**

Halmashauri ya Jiji la Dodoma ipo makini katika kutekeleza mikakati mbalimbali ya kitaifa ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira, ukiwepo mkakati wa kuhifadhi ardhi na vyanzo vya maji unaotaka kila wilaya kupanda miti million moja na nusu kila mwaka. Halmashauri kwa kushirikiana na na wadau mbalimbali wakiwemo TASAF, TFS na taasisi mbalimbali wameweza kupanda miti katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma kama vile chanzo cha maji Nzakwe, Chuo kikuu UDOM. Msitu wa Mahomanyika, kwenye makazi taasisi mbalimbali, kandokando ya barabara na maeneo ya wazi.

**Ndugu mgeni rasmi,**

Viongozi wa ngazi mbalimbali wamekuwa msitari wa mbele kuhamasisha utekelezaji wa zoezi hili akiwemo Mhe. Makamu wa Rais Mama Samia Hassan Suluhu aliyezindua kampeni ya kuifanya Dodoma kuwa ya kijani mnamo tarehe 21/12/2017 ambapo ilipandwa jumla ya miti 2,300 katika chanzo cha maji Nzakwe ambayo ilitolewa na TFS, Mheshimiwa mkuu wa mkoa wa Dodoma Mhe. Binilith Mahenge ambaye aliongoza zoezi la upandaji miti 1000 katika msitu wa Mahomanyika mnamo tarehe 08/02/2018 ambayo ilitolewa na mradi wa TASAF na Mkuu wa chuo kikuu cha UDOM aliyewaongoza wanafunzi kupanda miti takriban 10,000 ambayo ilitolewa na halmashauri ya Jiji la Dodoma.

**Ndugu mgeni rasmi,**

Viongozi hawa pamoja na viongozi wengine katika ngazi ya wilaya wamefanyika chachu kubwa ya mafanikio ya ustawi wa misitu na uoto kwa ujumla ndani ya Jiji la Dodoma na kuifanya Dodoma kuwa ya kuvutia hasa wakati huu muhimu wa ofisi za serikali kuamia makao makuu ya nchi yetu Jiji la Dodoma. Halmashauri ya

Jiji ikihusisha ofisi ya mkurugenzi inatoa pongezi  nyingi kwa Viongozi wote wanaotuhamasisha na kutuunga mkono kwenye kampeni hii muhimu kiwilaya kimkoa na kitaifa kwa ujumla.

**Ndugu mgeni rasmi,**

Jumla ya miche ya miti  iliyopandwa ndani ya Jiji letu  kwa kipindi cha miaka miwili ni 1,010,490 kuanzia kampeni ya kuifanya Dodoma ya Kijani ilipozinduliwa mwaka 2017 (Miti 593,918 kutoka Halmashauri, 414,272 kutoka TASAF na 2,300 kutoka TFS). Kati ya miti hii jumla ya miti 911,994 ilipandwa mwaka 2017/18 na jumla ya miti 98,496 kwa mwaka huu wa 2018/19 imeshapandwa mpaka sasa hivi, lakini bado upandaji wa miti unaendelea kutokana na mvua zinazonyesha kusuasua. Ofisi inaendelea kupokea maombi ya miti kutoka kwa wakazi na taasisi mbalimbali kulingana na uhitaji wao. Miche hii inagawiwa kwa wadau mbalimbali zikiwemo taasisi na watu binafsi ili ipandwe kwenye maeneo yaliyoathirika na yasiyo na miti. Miti mingi iliyopandwa inaendelea kukua vizuri.

**Ndugu mgeni rasmi,**

Jitihada zote hizi ni katika harakati za kufikia lengo la kutekeleza mkakati wa kitaifa wa kila wilaya kupanda miti milioni moja na nusu pamoja kuitekeleza programu ya kuifanya Dodoma kuwa ya kijani.

**Ndugu mgeni rasmi,**

Halmashauri ya jiji la Dodoma, imeweka mkazo katika upandaji miti, uboreshaji wa mandhari,uhifadhi wa misitu  na uoto wa asili kwenye vilima vyote vilivyomo ndani ya jiji na kuzuia shughuli zote za ki-binadamu zinazoharibu mazingira kwenye maeneo hayo kufanyika ikiwemo ukataji wa miti, uchomaji mkaa, uchungaji mifugo, kuzuia kilimo katika vilima na miteremko mikali na kuhimiza wakulima kubakiza miti mashambani (kisiki hai) kwa ajili ya kuongeza rutuba mashambani, kupata kivuli na kuzuia upepo mkali.

**CHANGAMOTO**

**Ndugu mgeni rasmi,**

Pamoja na mafanikio hayo, jitihada hizi zinakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

1. Athari za mabadiliko ya tabianchi za majira na viwango vya mvua kubadilikabadilika. Hali hii imechangia baadhi ya miti iliyopandwa kukauka kutokana na mvua kidogo na ukame wa muda mrefu. Pia imesababisha kuahirisha siku ya upandaji miti kitaifa tukijaribu kuendana na majira ya mvua.

2. Baadhi ya watu wenye mifugo kuchunga mifugo yao kiholela na kusababisha miti inayokua kukanyagwa, kuvunjwa na kuliwa na mifugo na kupelekea miti kushindwa kustawi vizuri.

3. Baadhi ya wananchi wanaopakana na hifadhi za misitu kuvamia maeneo hayo kwa nia ya kuanzisha mashamba, na kukata mikaa hali inayosababisha miti mingi ya asili kukatwa.

4. Utegemezi mkubwa wa jamii kwenye nishati ya kuni na mkaa kwa sababu ya kipato kidogo katika jamii ya Dodoma hali ianayopelekea kushindwa kumudu matumizi ya nishati mbadala.

**UTATUZI WA CHANGAMOTO**

1. Ofisi ya halmashauri ya Jiji la Dodoma imetoa elimu ya upandaji miti kulingana na majira ya mvua katika kata 41 za halmashauri ya Jiji na kuhamasisha upandaji miti kuanzia kwenye ngazi ya kaya taasisi na uanzishwaji wa mashamba ya miti kwa mitaa yenye maeneo makubwa.

2. Kuhamasisha upandaji miti ufanyike kwa wingi mashuleni na kila mwanafunzi akabidhiwe mti awajibike kuutunza hata kama ni kwa kuleta maji kutoka majumbani kwao.

3. Sheria ndogo za utunzaji na usimamizi wa Mazingira za Jiji la Dodoma zimesambazwa katika kata na mitaa ili kudhibiti mifugo inayokula miti inayokua na uvamizi wa jamii kwenye misitu ya asili.

4. Kudhibiti ukataji miti ovyo bila ya kibali cha Afisa mwidhiniwa kutoka Jiji.
5. Halmashauri imehamasisha wadau wa nishati mbadala kufikisha huduma kwa jamii zilizo mbali na mjini ambazo zimekuwa chachu ya uharibifu wa misitu ya asili.Taasisi ya MIGESADO na Chololo eco village wametoa mchango mkubwa sana katika kupeleka elimu ya matumizi ya biogas, majiko banifu, na majiko yasiyotumia mazao ya misitu kama vile pumba za mpunga kwa wakazi ikihusisha kata za Hombolo na Kikombo.
6. Halmashauri inahamasisha jamii kufanya shughuli mbadala za kuendeleza misitu za kujipatia kipato kama vile ufugaji nyuki na uanzishwaji wa vitalu vya miche ya miti ili kusogeza huduma ya upatikanaji wa miche karibu na jamii.